

DUNIA SI TAMBARA BOVU

1. Kwamba dunia kachara, i kama tambara bovu,
Ni mawazo chaparara, yamekosa welekevu,
Dunia kitu imara, ni mawazo maangavu,
Dunia ni yenye nguvu, hakuna aiwezae.
2. Hakuna aiwezae, dunia ni yenye nguvu,
Hakuna ajitapae, walojifanya ni ndovu,
Imewaponda jangae, wajanja na wapumbavu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki aiwezae.
3. Wako wapi Mafarao, kwa kani wachachamavu,
Walojidai ni wao, kila hali wakomavu,
Wenye masime na ngao, wamepurwa kama mavu,
Dunia ni yenye nguvu, hakuna aiwezae.
4. Pulika Habibu Shindo, usiwe mnyong'onyevu,
Hitila mwenye vishindo, alopura watu ndovu,
Kwa dunia zake nyundo, amesagwa sawa jivu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki aiwezae.
5. Wa wapi walojikweza, kutesa na maonevu,
Dunia waloshangaza, kwa nguvu na upotovu,
Dunia imewameza, wao na yao mafuvu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki wa kuiweza.
6. Wako wapi wenye sifa, palipo usuluhivu,
Wakaingiza maafa, kwa nyoyo za ukativu,
Hao! Wote wamekufa, si kwamba ni walemavu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki aiwezae.
7. Dunia kweli ni kongwe, kwa umuri ni komavu,
Juu ya hivyo magangwe, huwanasa kama wavu,
Na ajaribu agongwe, asemae ana mbavu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki aishindae.
8. Tambara bovu ni wewe, mwenye umbo tepetevu,
Jambo hili lielewe, jiandae kwa wokovu,
Mimi nawe tukatiwe, Firidaua angavu,
Dunia ni yenye nguvu, hazuki wa kuishinda.
9. Kaditamati shairi, dunia kamwe si chovu,
Na wala usifikiri, sawa na mti mkavu,
Imeshameza dahari, kwa nguvu si kwa uvivu,
Dunia ni yenye nguvu, hushindwa kwa aumbae.

Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)
Kinondoni-Shamba
DAR ES SALAAM
Tanzania.